

Ebrahim Hussein

1980 (1967)

WAKATI UKUTA

Nairobi: East African Publishing House

Nacherzählt von

Lourenco Noronha

Mzee Baruti¹

Lektor (1974-2009) für Swahili-Literatur

am

Institut für Afrikawissenschaften

der Universität Wien

Taaluma ya Bara la Afrika

Chuo Kikuu cha Vienna

Stand: November 2008

¹ *Ndilo jina nililolipewa shuleni Tanzania 1961-1972.*

Widmung
Kutabaruku

Nawashukuru walimu wangu katika
Idara ya P.W.D., Dar es Salaam, 1950-1953
pamoja na wanafunzi wa
Forodhani (St. Joseph's) Secondary School, Dar es Salaam, 1961-1968
na
Sangu Secondary School, Mbeya, 1969-1972
walionifunulia siri (mbinu) za lugha ya Kiswahili

al-hamdu li-llahi
subhanahu wa-ta'ala

Vorwort
Dibaji

Angeregt wurden diese didaktischen Unterlagen von Studierenden am Institut für Afrikawissenschaften der Universität Wien.

Die deutschsprachigen Teile wurden von Dr. Franz Rader korrigiert; dieser hat während seiner Tätigkeit an der Österreichischen Botschaft in Nairobi meine Berufung nach Wien gefördert. Für beides bin ich ihm dankbar.

Lourenco Noronha
Ungargasse 38/431
A-1030 Wien
E-mail: noronha@gmx.at

Leitgedanke
Dhamira Kuu

Mzee Juma:

“ Wakati ukuta – ukipigana nao utaumia mwenyewe.”

Ebrahim Hussein
Wakati Ukuta
Nairobi: EAPH
Uk. 17

1. Einleitung
Utangulizi

1.1. Autor: biographische Notizen
Wasifu ya Mtunzi

Ebrahim Hussein wurde 1943 in Lindi geboren. Er besuchte die *Aga Khan Secondary School* in Dar-es-Salaam, studierte von 1966 bis 1969 Literatur, Französisch, Soziologie und Theaterwissenschaft an der dortigen Universität. 1969 war er wissenschaftlicher Assistent am *Department of Theatre, Arts, and Music* der Universität Dar-es-Salaam und seit 1970 wissenschaftlicher Aspirant an der Humboldt-Universität zu Berlin, wo er in Theaterwissenschaft promovierte. Seine Dissertation, datiert 1971, trägt den Titel The Development of Drama in East Africa. 1978 kehrte er an die Universität Dar-es-Salaam zurück und lehrte am *Department of Theatre, Arts, and Music*.²

1.2. Thematische Einführung
Kiini (dhamira, dhana, mada, wanda/ma-) maalum

In Wakati Ukuta bzw. Wakati ni Ukuta (Die Zeit ist eine Wand) greift Ebrahim Hussein in fünf rasch aufeinander folgenden Szenen das Thema "Emanzipierte Mädchen in der afrikanischen Gesellschaft" der 70er-Jahre des vergangenen Jahrhunderts in Tansania auf. Wenn ich mich richtig erinnern kann, wurde dieser Theatertext von der *Jangwani Girls' Secondary School* (früher: *Indian Girls' Secondary School*) in Dar-es-Salaam uraufgeführt. Auch in den 80er-Jahren war es ein beliebter und viel diskutierter Theatertext.

Der Ausgangspunkt für den Konflikt zwischen dem Mädchen Tatu und ihren Eltern liegt in ihrem Wunsch, mit einem jungem Mann Swai ins Kino zu gehen, ein Umstand, den die sittenstrenge islamische Gesellschaft nicht akzeptiert. Tatu und Swai sind der Ansicht, daß gesellschaftliche Normen veränderlich sind und den Zeitumständen angepaßt werden sollen. Die Mutter von Tatu dagegen hält an einem starren Gefüge fest. Ihre Tochter soll so leben und so heiraten, wie sie es dereinst getan hat.

Ich nehme an, daß die Ansicht des Autors der Auffassung von Mzee Juma entspricht, nämlich das Verhalten einer Generation muß nicht identisch mit dem der vorherigen Generation sein. Es fällt mir aber schwer, Mzee Jumas Aussage: „*Wakati³ ukuta – ukipigana nao utaumia mwenyewe*“ (Uk. 17) auszulegen.

Ich nehme an, dass Zeit für ihn eine Wand ist. Schieben und verschieben kann man sie nicht. Gegen sie zu prahlen bringt schlimme Folgen. Sie zu umgehen ist nicht möglich. Im gleichen Gespräch sagt er auch, dass er und seine Frau sich nicht wie ihre Vorfahren verhalten und ihre Kinder anders leben werden als sie selbst.

Kiswahili kennt zwei⁴ Begriffe für Zeit, nämlich „*muda*“ und „*wakati*“. „*Muda*“ ist eine „bestimmte Zeitspanne“ im Sinne von „Ich arbeite acht Stunden täglich.“ „*Wakati*“ ist

2 Weitere Information: Internet.

3 Kiswahili und Alt-Griechisch sind nicht verwandt. Ich möchte es mir trotzdem erlauben, die Begriffe *Chronos* und *Kairos* zu erwähnen.

4 Begriffe im Umfeld von „Zeit“ sind: *aushi, faragha, juma, kipindi, kitambo, maisha, majira, muhula, mwezi, nafasi, nukta, saa, wasaa, zamani*.

eine „bestimmte Zeit“ bzw. eine Reihenfolge von Handlungen im Sinne von „Alles hat seine Zeit.“⁵ etwa in „*Mimi husoma, hufanya kazi, hula, hulala wakati wake*“. „*Wakati*“ hat auch ein Mehrzahl in Kiswahili, nämlich „*Nyakati*.“ Die Römer pflegten zu sagen: „*Tempus fugit dum stare videtur*“. Die Zeit bleibt nicht stehen, d.h. Ein Ereignis folgt dem anderen. Die Griechen kennen die Begriffe *chronos* und *kairos*. Ich habe dem Eindruck, dass Tatu und ihre Mutter zur gleichen Zeit leben und doch in anderen Zeiten. Das ist Ebrahim Hussein's Begriff „*Wakati*“ .

Aus den Diskussionen mit Schülerinnen und Schülern nach einer Aufführung gewann ich den Eindruck, daß es nicht angebracht ist, herkömmliche Strukturen abzuschaffen, ohne einen funktionierenden Ersatz anzubieten.

Kichekesho, eine Variante von „Volksbelustigung“ wird in Swahili-Theatertexten eingebaut. Gewöhnlich kommen in diesem Kontext Inder mit mangelnden Sprachkompetenz, die asozial dargestellt werden oder „Tratschweiber“ vor.

1.3. Literaturhinweise.

Marejeo

Die Zahlen in Klammern entsprechen der Signatur der Fachbibliothek der Afrikawissenschaften und Orientalistik der Universität Wien.

1.3.1. Primärliteratur

- Fiebach, Joakim (ed.). 1974. Stücke Afrikas (In deutscher Übersetzung: Hussein, Ebrahim. Kinjeketile. Ramadhani, John. Streik in Mazinde). Henschel Verlag.
- Hussein, Ebrahim. 1981 (1969). Kinjeketile. Nairobi: OUP. 49pp. (B.8.9.26.).
- Hussein, Ebrahim. 1970. Michezo ya Kuigiza (Wakati Ukuta & Alikiona). Nairobi: EAPH. 64pp. (B.8.9.7.).
- Hussein, Ebrahim. 1987 (1971). Mashetani. Dar es Salaam: OUP. 57pp. (B.8.9.27-1.).
- Hussein, Ebrahim. 1975 (1971). Wakati Ukuta. Nairobi: EAPH. 41pp. (B.8.9.4.).
- Hussein, Ebrahim. 1976. Jogoo Kijijini & Ngao ya Jadi. Nairobi: OUP. 50pp. (B.8.9.55.).
- Hussein, Ebrahim. 1984 (1980). Arusi. Nairobi: OUP. 50 pp. (B.8.9.25.).
- Hussein, Ebrahim. 1982. Jambo la Maana. Dar es Salaam: Africana Publishers. 28pp. (B.8.14.20.).

1.3.2. Sekundärliteratur

- Hussein, Ebrahim N. 1980. „Traditional African Theatre“, in: Schild, Ulla. The East African Experience. Berlin: Reimer, S. 35-53. (S.6.6.1.).
- King'ei, Godfrey K. 1987. „Usanifu wa Lugha katika Uandishi wa Ebrahim Hussein“, in: Mulika. Dar es Salaam: IKR. 19, S. 19-35. (Z.1.11.19.).
- Mmbago, Nathaniel. „Msingi ya Michezo za Kuigiza: Michezo ya Ebrahim Hussein“, in: Mulika. Dar es Salaam: IKR.
- Mugo, Micere Githae. 1976. „Gerishon Ngugi, Penina Muhando and Ebrahim Hussein. Plays in Swahili“, in: African Literature Today. London: Heinemann. 8, S. 137-141. (Z.3.1.8.).
- Sengo, Tigiti. 1975. „Ebrahim Hussein. Mwandishi wa Michezo ya Kuigiza“, in: Hisi
- 5 Eine Teewerbung lautet: „*Wakati wote chai*.“

Zetu. Dar es Salaam: IKR. 2, S. 58-95. (Z.1.35-2.).

2. Texte *Matini*

2.1. Personen *Wahusika*

Tatu: Mädchen, etwa 21 Jahre jung. Hat eine Schulausbildung.

Juma: Tatus Vater, etwa 40-50 Jahre alt. Er hat keine Schule besucht.

Asha: Tatus Mutter, etwa 40-41 Jahre alt. Sie hat keine Schule besucht.

Kristina:

Eine Freundin Tatus, etwa 20 Jahre jung.

Swai: Tatus Freund, etwa 21 Jahre jung.

Pili: Swais Freundin, etwa 18 Jahre jung.

Bibi

1,2,3: „Tratsch-Weiber“ im Alter von 43 bis 50 Jahren.

2.2. Der Theatertext *Tamthilia*

2.2.1. Onyesho la Kwanza

Asha, die Mutter Tatus befindet sich im Wohnzimmer ihres Hauses. Es gibt wenige Sachen in diesem Zimmer: einen Tisch mit Radio, einen Wasserkrug, Trinkgläser und eine Couch. Die hintere Türe führt zum Innenhof. Die Eingangstüre liegt auf der linken Seite. Asha sitzt im Wohnzimmer und flechtet Matten aus Palmblättern, sie spricht mit ihrer Tochter Tatu.

Mama Tatu: (Anamtazama bila kupendezwa. Anasema huku anasuka ukili) Hmm. Hiyo kanzu imezidi tena. Si unatembea uchi hivyo. Fupi, fupi, imekubana, imekubana. Ndio uambiwe nini? Mzungu sana!

Tatu: Mama watoto wanavaa hivi hivi siku hizi (ananung'unika).

Mama: Hm. Haya sisi yetu macho tu. Maana husikizi tena. Umekuwa mkubwa, siwezi kukupiga. Basi haya utakavyo tu (Kimya).

Tatu: Maa (Kwa hofu kidogo).

Mama: Sema tu, nakusikia.

Tatu: Ahema. Nataka ruhusa kwenda sinema.

Mama: Sinema gani?

Tatu: Empress⁶.

Mama: Basi si bado? Leo ndio kwanza Ijumaa; "Lady Show"⁷ Jumapili.

Tatu: Nataka kwenda leo usiku.

Mama: Toka lini ukaenda sinema usiku? Siku zote unakwenda Jumapili mchana. Mchana sikukatazi, lakini usiku hapana, hapana, hata kidogo. Kwanza pesa za kukupa wewe kila Jumapili ziko wapi? Baba yako hali yake unaijua. Kila siku hapa analalamika kodi zimekuwa nyingi. Nawe unamsikia. Kodi ya kichwa, kodi ya miguu, kodi ya uzee, kodi ya mapato, kodi ya wafanya kazi, kodi, kodi, ilee!

6 Ein populäres Kino nahe dem Askari-Denkmal, das damals Herrn Fernandes, einem Inder aus Goa gehörte.

7 „Ladies' Show“ ist in Indien üblich und bedeutet eine Kinovorführung nur für Mädchen und Frauen, gewöhnlich sonntags nachmittag.

Nawe unataka sinema. Pesa zenyewe ziko wapi?

Tatu: Mie sitaki pesa, nipe ruhusa tu. Swai atanichukua sinema. (*Ma tatu amestuka. Anamtazama Tatu. Anarudia kusuka ukili wake*) (*Kimya*)

Tatu: Ma, atakuja sasa hivi. Jee nende (niende)? (*Kimya*)

Mama: (*Pole pole*) na huyu Swai ndio nani?

Tatu: Mtoto mmoja Swai Hamisi. Najuana nae.

Mama: Mwanamume?

Tatu: (*Anaitikia kwa kichwa*)

Mama: Nae anakuchukua sinema – Na kwa nini yeye akulipe sinema? Anakujuaje? Baba yako? Au nani? (*Anaacha kusuka*) (*Kimya*)

Mama: (*Sauti ya juu*) Nijibu! Wewe unafikiri, anapata taabu hii yote ya kukuchukua sinema kwa nini, eh? Wewe mwana mzima sasa huwezi kufikiria?

Tatu: Mama ingekuwa kuna jambo lolote baya tusingetaka ruhusa. Swai ni rafiki tu.

Mama: “Hakuna urafiki baina ya mtoto wa kiume na mwanamwali, hata kidogo. Uwongo. Usitudanganye. Hivi unaniona mjinga sana, eh?” (*Uk. 9-11*).

Als Tatu ihrer Mutter zu erklären versucht, daß heutzutage junge Mädchen mit ihren Freunden ausgehen, lehnt die Mutter das Vorhaben ab.

Mama: “Sio uzungu? Ndio kuiga uzungu tena. Basi sisi si Wazungu. Mzungu na Mwafrika mbali mbali. Wao hawana haya, anaweza kwenda na mume huyu na mume yule isiwe kitu. Hivi ndivyo kikwao. Ndivyo walivyolelewa. Haya mgeni kwetu. Usifikiri nakuchukua au kubughudhi. Wewe leo nenda na Swai, macho yanakufuata, midomo inanong’ona. Kesho na Musa, siku ya pili na Saidi, watu wanakutazama. Hata ingalikuwa kama unavyosema ni rafiki tu. Waafrika tulivyo hatutafikiri hivyo. Utaharibu jina lako bure.” (*Uk. 12*).

Tatu antwortet, daß sie nicht interessiert sei zu wissen, was die Leute reden.

Mama: “Mimi najali – sitaki aibu mimi. Unalofanya wewe sio aibu yako tu, bali ya wote, mimi, baba yako, ukoo mzima. Mimi nimelelewa na wazee wangu, nilipokuwa mkubwa wakanipa mume. Sikumjua, hakunijua, lakini mpaka sasa tunakaa vema. Nami nitakufanyia hivyo vivyo. Mpaka nikupe nyumba⁸ yako halafu hapo tena shauri yako. Kama huyu Swai anakupenda mwache alete posa.” (*Uk. 12*).

Als Tatu ihr erklärt, daß die Zeiten sich geändert haben, wird die Mutter ungehalten und verbietet ihr schlicht den Ausgang mit Swai. Tatu gibt aber nicht nach.

Tatu: Lakini Ma wakati⁹ umebadilika sa...

Mama: (*Sauti kali*) Sitaki kusikia. Akija hapa ... huyu nani sijui, mwambie huwezi kwenda. (*Mkali*) Tena nakuambia kweli. Maana nakuona kichwa chako kinakua kikubwa sasa. Unaweza kunijibu. Tulivyolelewa sisi hatuwezi kumjibu mzee wetu. Basi leo huendi mahali. Nikuone uinue mguu tu.

Tatu: (*Ananung’unika*) Aaa mie nitakwenda Ma.

Mama: Tatu nakuambia, tena nakuambia eeh! Hunijibu. Wewe na huyo mwanamume

8 Verheiraten

9 Wenn Zeit eine Reihenfolge von Handlungen, Ereignisse ist, dann ist die gegenwärtige Lage (Situation) anders, als jene zu der Zeit, als die Mutter Tatus jung war.

wako nitakufukuzeni (nitawafukuzeni ninyi) nyote hapa ukiniletea ujuba wako.
(Uk. 12).

Swai klopft an. Die Mutter erkündigt sich nach dem Wunsch des Gastes und teilt ihm eiligst mit, daß Tatu nicht zuhause sei, da meldet sich diese.

Tatu: Nipo, karibuni.

Mama: (Kwa sauti ya chini lakini kwa ukali) Mimi nakuambia ukitoka nae (naye) usirudi nyumba hii.

Swai: (Anaingia) Hodi tena. Shikamoo Ma.

Mama: Marahaba. Tatu hawezi kwenda sinema. Ana kazi.

Swai: Lakini, aliniambia ...

Mama: Ah! Wewe usifuate alichokuambia. Mie nakuambia haendi. Kwaheri.
(Anamfungulia mlango).

Tatu: Ma huwezi kumfukuza mgeni wangu namna hii.

Mama: Siwezi! Unaniambia nini? Siwezi. Nitakuonyesha basi kama naweza.
(Analikamata shati la Swai kwa nyuma) Toka, toka, toka.

Tatu: (Tatu anaingilia kumshika Ma) Mama!

Mama: Ho! Unataka kupigana na mimi sasa!

Tatu: Sio nagombana nawe, lakini si haki kumfukuza mgeni.

Mama: Usie (usiwe) na fadhila we, huna adabu na wewe toka. Tokeni, tokeni. Nyote sitaki kukuoneni – (Anawafukuza, anamsukuma Tatu) Toka, tena usirudi, tena – sitaki kukuona machoni mwangu. (Anaufunga mlango kwa gadhabu. Anannung'unika) Alaa kwa nini? Watoto si watoto. Hawaogopi wazee. Afadhali kutozaa mtu ukashukuru Mungu. Wallahi¹⁰! Kuliko kupata mtoto namna hii.
(Uk. 13-14).

Sie flicht ihre Matte weiter. Der Vater¹¹ kommt herein. Er erkündigt sich nach ihrem Befinden, denn er merkt, daß irgend etwas nicht stimmt.

Mama: Mtoto – huyu mtoto wako¹². Mtoto hana adabu hana heshima. Basi leo nimemfukuza nyumbani hapa. Mwache atokomee huko.

Baba: Una maana kwamba ... eh ... sijaelewa. Wewe ... Ah. Umemfukuza Tatu, maana yake asije hapa tena?

Mama: Ndiyo sitaki kumtia machoni tena; sina mtoto mie.

Baba: Sasa kumfukuza huku (Anakuja juu) katika akili yako ende (aende) wapi? Acha kazi hiyo unayofanya (Anauchukua ukili aliokuwa akiutengenza anautupa) Nijibu. Na nini kikubwa alichokifanya hata umemfukuza hapa. Sema.

Mama: Mtoto wako kanitukana na kutaka kunipiga hapa.

Baba: Hata kidogo, hata kidogo, Tatu hawezi kukutukana wewe.

Mama: Hawezi, basi leo kaweza (akaweza).

Baba: Alisema nini?

Mama: Alisema nini? Uliza kafanya (akafanya) nini.

Baba: Sasa husemi.

Mama: Basi mtoto wako leo kaniletea (akaniletea) mwanamume wake hapa hapa ndani.

10 "Im Namen Gottes!" „By God!“, eine Eidesformel, die bei den Wa-Swahili üblich ist.

11 In der Swahili-Literatur wird gewöhnlich der Vater als streng und manchmal als jähzornig dargestellt. Die Mutter ist gewöhnlich versöhnend, ein ruhender Punkt.

12 Sie übernimmt keine Verantwortung für Tatu.

(Uk. 15-16).

Der Vater von Tatu setzt sich. Er möchte die schwierige Lage mit seiner Frau in Ruhe besprechen.

Baba: Hapana, sisemi hivyo. Sisemi ungemwachia (a)ende nae, lakini usingemfukuza nyumbani. (Kimya). Mke wangu (Anamuelezea) mambo namna hii hayataki hasira - bali busara, siasa¹³. Mwarabu alitutawala sisi, na sisi tukafuata tabia zake na mila zake. Nitazame mie navaa kofia na kanzu. Kwani jadi yangu mimi ni kofia na kanzu - au asili yako wewe, watani wako, walivaa buibui au mtandio? Sisi hatukuwa kama wazee wetu. Basi na hawa watoto wetu vilevile. Wanasoma kizungu, tunawavalisha kizungu, wanakwenda shuleni kusoma kizungu - Na wataiga kizungu katika kusema, mavazi, mila hata na tabia. Sisi tunaona mabaya, wao wanaona mazuri. Hakuna mtu anayeweza kushindana na wakati. Wakati ukuta, ukipigana nao utaumia mwenyewe. Tutagombana na watoto wetu bure. Hivi tutawakosea watoto wetu. Letu tuwachunge tujitahidi kama tunavyoweza. Tukaze, lakini tukiona kamba karibu kukatika, tulegeze. Naamini katika akili yangu kama ungalimueleza Tatu kwa utaratibu angalielewa. (Uk. 17).

Die Mutter fragt, ob sie einen Fehler begangen habe.

Baba: Hukukosa mke wangu katika kumkataza. Wala Tatu hakukosa.

Mama: Sasa?

Baba: Ni wakati tu. Wakati sio sawa. (Anaonyesha ana fikira kubwa) Tatu amesoma vitabu vya kizungu, ameona mtoto wa kike na kiume wanatembea wanakwenda dansini au sinema. Wanapendana mwisho wanaoana. Sio Tatu tu, watoto makamo yao wote. Na wao wanataka kuiga yale. Wakati wa kufanya haya utakuja, lakini sasa hivi bado. Sasa yeye kutaka kuwa katika wa kwanza kufanya haya anagombana na wakati. Anataka uje upesi na sisi tunagombana na wakati, tunataka usije. Hapa ndio (hapo ndipo) ulipo ugomvi wetu. (Kimya). (Uk. 19).

Der Vater weiß nun, daß seine Tochter nicht zurückkommen wird. Er möchte jedoch herausfinden, wo sie sich befindet.

2.2.2. Onyesho la Pili

Mzee Juma hält sich im gleichen Wohnzimmer auf. Er hat ein Leibchen mit Ärmel und ein weißes Lendentuch an. Er trägt keine Mütze. Er sitzt auf einem Sessel, hat sich nach vorne gebeugt und denkt nach. Er blickt auf seine Uhr. Er schaltet das Radio ein, hört die Nachrichten und schaltet es wieder aus. Seine Frau kommt und meldet, daß das Essen bereit steht. Er hat aber keinen Appetit. Es ist schon der zweite Tag, daß er seine Tochter sucht. Er findet sie nicht. Woher soll er nun Lust aufs Essen haben?

Inzwischen klopft jemand an die Tür. Mzee Juma zieht sich rasch um und öffnet die Türe. Kristina kommt herein.

¹³ Die ursprüngliche Bedeutung von „siasa“ ist: “Orderliness, gentleness, carefulness, politics, and as an adverb gently, with care, in an orderly fashion“ F. Johnson. 1939. A Swahili-English Dictionary. OUP. S. 428.

Kristina: Shikamoo!

Baba: Marahaba, marahaba, pita.

Kristina: Jee hii ndio (ndiyo) nyumba ya Bwana Juma?

Baba: Ehee hasa-a mimi ndio (ndiye) Bwana Juma – Pita basi pita kaa juu ya kiti – Tusameheane, viti vyenyewe ndio (ndiyo) viti jina tu – lakini ...

Kristina: Ah inatosha tu mzee. Hata sijui nianze vipi maana ...

Baba: Ah anza tu – anza tu – usiogope wewe sema tu.

Kristina: Mimi ni rafiki yake Tatu ...

Baba: (*Anaonyesha hamu kubwa ya kujua zaidi na anasema upesi upesi*) Tatu? – yuko wapi? (*Anamwita mkewe*) Mama Tatu – njoo – eh eh umemwacha wapi ... yuko wapi? (*Anainuka anakwenda mlangoni na kutoka nje*) sasa anaogopa kuja ndani? Hatumpigi (*Anafungua mlango anaita*) Tatu, Tatu – yuko wapi? (*Kimya. Anarudi. Ma Tatu ametokea mlango wa kuendea ndani pole pole amesimama karibu na kiti – ameshika sahani*)

Baba: Mbona hayupo. (*Anamwuliza Kristina*)

Kristina: Ehe.

Baba: Sasa unaogopa nini? Ungejua tulivyomtafuta, jana usiku hatukulala, leo sikwenda hata sokoni kufanya biashara. Usingizi umetupaa, chakula hakitushuki. Najua amekuambia usituambie alipo – lakini sharti ufahamu alipo – lakini sharti ufahamu sisi wazee wake –

Kristina: Mie ameniambia kama mmemfukuza alipokuja kwangu kulala.

Mama: Amfukuze nani? Kuna mzee akamfukuza mtoto wake? (*Juma anamtazama mkewe kwa muda kidogo ambaye anangusha uso wake na kutazama chini kwa haya*). (*Uk. 20-22*).

Mzee Juma erkundigt sich nach Kristinas Herkunft. Sie sagt, daß sie in Moshi¹⁴ aufgewachsen ist, wo ihre Eltern wohnen. Sie lebt aber jetzt in Dar-es-Salaam. Sie äußert ihre Zweifel, daß Tatu je nach Hause zurückkehren werde.

Kristina: Sifikiri kama atarudi tena hapa.

Baba: Kwa nini?

Kristina: Swai na Tatu wameoana leo –. (*Uk. 23*).

Der Mutter wird schwindlig. Sie lässt den Teller aus ihrer Hand fallen und sucht eine Stütze. Der Vater heißt sie sich zu setzen. Es kommt zu einem Gespräch zwischen Kristina und Mzee Juma.

Baba: Tatu na Swai wameoana leo – ndio (ndiyo) ulivyosema – au ...

Kristina: Ndivyo nilivyosema. (*Kimya*)

Baba: Kuoana huku wameoanaje – Nani alitoa ruhusa hii?

Kristina: Wameoana kwa Area Commissioner.

Baba: La haula. (*Anainuka*) Haya basi imekuwa sasa hata mtoto wako mwenyewe mtu huna idhini nae (naye), balaa tena.

Kristina: Mtoto vile vile ni mtu, sio kama nakuvunjia heshima, lakini watu wa humu pwani mnafanya mtoto kama mzigo, hasa mtoto wa kike. Mnamfutika futika na kumficha. Akitaka kwenda huku hapana, akitaka kufanya hiki hana ruhusa. Hata mume mnamchagulia nyie – Watoto wa sasa haya wanaona dhiki.

Baba: Sisi wajinga, hatukusoma lakini si wajinga hivyo. Haya mambo kweli

¹⁴ Die *Wachagga* von Moshi haben einen hohen Bildungsstandard (nach westlichem Muster) und gelten als sehr aufgeschlossen.

yalikuwepo zamani lakini yanakufa. Haya mambo haya, hayafi kwa siku moja, wala kwa mwaka mmoja. Sisi ingawa tuko nyuma lakini sio nyuma hivyo – Huyu Swai angekuja, angemposa sisi tungemuozia. Lakini hivi alivyofanya kenda katutukanisha (huenda akatutukanisha) sisi wote. Watu wa mlima nyie hamuwezi kufahamu haya.

Kristina: Lakini Swai¹⁵ kasema si mnagalimkubali, kwa ajili hana kitu na mtu wa bara ... Kwa hiyo wakaona afadhali ...

Baba: Alaa kwani ... ah! Basi mimi nilifikiri. ... yeye aliniambia ... (*Uk. 24-25*).

Mzee Juma nimmt die Heirat zur Kenntnis, fügt aber hinzu: „Mtoto akililia kisu, mpe!“ Er erkundigt sich nach dem Status von Swai.

Kristina: Yeye ni karani. Alifeli darasa la 12 mwaka juzi akaanza kazi.

Baba: Hmmm. Haya –

Kristina: Mzee nasikitika sana tena kweli kabisa sikujua kama mambo yenyewe ndio hivyo. Mimi wameniambia vingine – kwa kweli hawakuniambia nije. Wao walinikataza lakini mimi niliona mtahangaika sana.

Baba: Ah hili si kosa lako. Sasa ndio hutaki kuniambia wanakaa wapi? Tazama leo kuna kuoana, kesho kuna kuachana. Je likitokea ala kutokea, Tatu atakwenda wapi? Basi haja yangu kumwambia tu, kuwa hapa ni pake, hii nyumba yake. (*Uk. 26*).

Er beauftragt Kristina, seiner Tochter Tatu mitzuteilen, daß er bereit ist, sie herzlich aufzunehmen, wenn sie zurückkäme. Kristina verabschiedet sich.

2.2.3. Onyesho la Tatu

Das Wohnzimmer bei Mzee Juma. Es ist niemand auf der Bühne. Man hört „Hodi“. Die Mutter Tatus betritt die Bühne.

Mama: (*Anatokeza mlangoni*) Karibu. (*Lakini anatamani aondoke*)

Bibi 1: Habari –

Mama: Nzuri tu – karibu -

Bibi 1: Ah hata sikai. (*Anakaa*) Hivi nimepita tu mara moja. Nakwenda zangu huko, lakini kiu kilinishika nikasema - ah nitaingia kwa Ma Tatu ninywe maji mara moja. Maana nyumba hii wenyeji - eh eh eh eh. (*Bibi Tatu anakwenda kuchota maji katika gudulia*).

Bibi 1: Ah si kumwita Tatu tu ataleta (*Mama Tatu amesimama tuli. Kuna kimya*). Una mtoto mzima unapata taabu ya nini?

Mama Tatu: Haya maji.

Bibi 1: (*Anapokea lakini hanywi maji*) eeh kabla sijasahau – nina salamu zake Tatu – nataka kumpa sijui ...

Mama: Je, ungependa soda ?

Bibi 1: Hapana – eh ilikuwa nakuuliza kitu – ah nini vile? Ah nimekumbuka, kweli, eti Tatu ... (*Hodi, hodi*) (*Bibi 1, anapopewa mgongo na Ma Tatu anaweka glass ya maji chini bila kunywa*).

Mama: Karibu.

Bibi 2: (*Ameingia*) Starehe.

Mama: Karibu, karibu, kaa.

15 Meines Erachtens ist Swai ein Familienname aus dem Kilimanjaro-Gebiet.

Bibi 2: Nilikuwa napita njia tu. Nikasema ah siku nyingi huyu bibi sijamwona – na jirani lazima kupitiana pitiana ...

Mama: Lakini si juzi tulionana vilevile.

Bibi 2: Ala hivi juzi vile – (*Anaona haya kugunduliwa*). Hodi, hodi.

Mama: Karibu.

Bibi 3 na 4: (*Wanaingia wanawake wawili. Wote wanajuana*)

Bibi 3: Heh, mara mko huku si – tulikuwa ... pamoja arusini?

Bibi 4: Habari Ma Tatu.

Mama: Mzima.

Bibi 4: Pole.

Bibi 1 na 2: Pole? (*pamoja*)

Bibi 1: Kwa nini? (*Anajidai hajui*)

Bibi 3: Ah babu we usijidai hukusikia – arusini kila mtu akisema hayo hayo.

Bibi 1: Ah sikusikia kitu. (*Aonyesha wazi kuwa anaogopa*)

Bibi 2: Ata (hata) mimi bibi iii (*Nae aonyesha mwongo*)

Bibi 4: Ah msalieni Mtume jamani.

Bibi 1: Kwani ningejua nifiche nini! – Si ningesema tu.

Bibi 3: Basi Tatu kamkimbua mama yake.

Bibi 1: Oh (*Anastuka*) Lo – ehe kenda wapi?

Bibi 4: Si katoroka na mwanamume wake.

Bibi 3: Po – Basi.

Bibi 3: Mimi nasikia lakini wameoana kwa Area Commissioner.

Bibi 1: Haya jamani! – masaibu.

Bibi 2: Masaibu, masaibu.

Bibi 3: Watoto wa siku hizi.

Bibi 4: Basi watoto bibi ... Watoto masaibu. Afadhali kukosa mtoto ... (*Pazia linafungwa huku wanasema.*) (*Uk. 28-31*).

Diese vier Frauen haben Ausreden genützt, um Mama Tatu auszufragen.

2.2.4. Onyesho la Nne

Drei Monate später. Tatu befindet sich in ihrer Wohnung. Sie macht das Bett. Swai stört sie bei der Arbeit. Er spricht davon, tanzen zu gehen, aber sie hat Sorgen mit dem Haushaltsgeld.

Swai: Leo, vaa kanzu yako nzuri tutakwenda katika marumba. (*Anacheza rumba*)

Tatu: Pesa zenyewe ziko wapi?

Swai: Umesahau –mwisho wa mwezi leo. (*anaendelea kucheza*). (*Kimya. Tatu anaendelea kutandika*) Jee mbona hivyo? Hupendi densi?

Tatu: Sio sipendi.

Swai: Tena?

Tatu: Hatuwezi kwenda. Pesa za watu hatujalipa - tuna madeni chungu nzima.

Swai: Tatalipa mwezi mwingine.

Tatu: Mwezi ule ulisema hivyo hivyo. Mshihiri yule anakuja hapa unajificha. Kodi ya nyumba - taa - maji. Jana nilipokwenda kaniambia kuwa mwezi huu kama hatukumlipa hatupi tena chakula. Haya sasa chakula bora au densi.

Swai: Ah hii adhabu tena - kula kulala, kula kulala - imekuwa si maisha haya tena. Zamani nikikaa kwa raha - sinema, densi, lakini sasa kazini, nyumbani, nyumbani, kazini. Mtu hajifurahishi hata kidogo. Najuta.

Tatu: Unajuta nini? (*Kimya*). Sema hicho unachojuta ni nini? Basi uliniolea (ya) nini kama unajuta.
Swai: Kwani nani kasema habari ya kuoa hapa?
Tatu: Si wewe hapo - umesema unajuta.
Swai: Sikusema hivyo.
Tatu: Umesema.
Swai: Sikusema hivyo, kama hata nikisema kwani itakuwa nini?
Tatu: Basi sikusema tu.
Swai: Haya basi nasema sasa - ninajuta. Nani ataweza maisha ya namna hii?
Tatu: Sasa uliniolea (ya) nini?
Swai: Nilikuoa nikikuonea huruma tu. Wazee wako wamekufukuza huko nyumbani - (*Hili limemchoma Tatu. Machozi yanamlenga - anajikingiza macho. Kimya*). (*Uk. 32-34*).

Swai bedauert seine Bemerkung. Er bittet sie um Verzeihung. Nach einem kurzen Gespräch einigen sie sich über Beträge für die Einkäufe, für die Schulden beim Araber, für die Hausmiete sowie für Wasser und Strom. Tatu geht einkaufen. Pili, Swais frühere Freundin klopft an.

Swai: Karibu, ingia tu, mlango haukufungwa. (*Anamwona Pili amevaa vizuri*) Oh Pili karibu, si kufikiri kama ... ah umekujaje huku. Kaa – mahali penyewe, eh eh, kama unavyoona.
Pili: Oh pazuri.
Swai: Pazuri hapana. Jee habari za siku nyingi.
Pili: Vizuri tu. Nimekuja kuwatazama bwana arusi mzima? (*Kwa dhihaka kama anamcheka*¹⁶)
Swai: Acha kunitania.
Pili: Ah nakutaniaje? Kwani hukuo. Tena kibamba unachokipenda.
Swai: Umeniudhikia?
Pili: Nikuudhikie? Kwa nini?
Swai: Labda utafikiri kuwa wewe nikiudanganya. (*Anajaribu kumshika, Pili anaondoka*).
Pili: Tena ukifanya nini? Huku mimi mjinga wako ukinidanganya lakini kwa kweli ... ukimpenda siti ...
Swai: Hayo si kweli ... unajua kama mimi kwa hakika nakupenda wewe.
Pili: Ha-ha-ha. (*Mlango unafunguka Tatu na Kristina wanaingia. Swai na Pili kwa sababu wanatazama upande mwingine hawawaoni*). Usinichekeshe Bwana unanipenda mimi. Je siti Tatu.
Swai: Tazama ... mimi sikatai kama nimemuoa Tatu, lakini ... unajua hatukufikiria. Wazee walipomfukuza nyumbani katika hasira tukaoana. Vile vile nilifikiri nampenda, lakini baada ya miezi mitatu hii ya dhiki nimetambua kuwa ... (*Anamfauata Pili, anataka kumkamata. Pili anamkimbia*.)
Pili: Ah hebu, ha! Ha! Ha! (*Wanamuona Tatu na Kristina. Wote wanatazamana – wamesimama tuli*.) (*Uk. 36-37*).

Pili ist weg. Swai, Tatu und Kristina stehen schweigend und ratlos da.

2.2.5. Onyesho la Tano

¹⁶ *Anacheka* = er/sie lacht, *anamcheka* = er/sie lacht ihn/sie aus.

Tatu sitzt an der Bettkante. Swai geht hin und her. Tatu versucht langsam etwas zu sagen, das sie schwer aussprechen kann. Aber dann kommt sie zur Sache.

Tatu: Naona ... mimi naona (*pole pole*) ... ingalikuwa bora ukaniacha¹⁷.

Swai: (*Angekuwa na haraka*) Nikuache?

Tatu: Ndio, uniache.

Swai: Maneno gani hayo – utakwenda wapi?

Tatu: Sijui, labda kwa wazee wangu kama watanisamehe niliyo *watendea*.

Swai: Wazee – wewe uliapa kama hutarudi.

Tatu: Nilikuwa mdogo. Nilifikiri kuwa nitaweza kuishi bila kutaka msaada wao. Nilidhani kuwa ... Nilidhani kuwa ...

Swai: Lakini (*Anakwenda kukaa mbele yake Tatu*) hata mwezi wa tatu haujafika toka kuoana, watu watafikiri nini? Najua kwa sababu gani unataka kurudi kwenu, kwa sababu ya Pili. Nimekuambia kuwa haitatokea tena. Nimekutaka msamaha, nimekuambia kama nimekosa – sasa nifanyeje? (*Tatu hamtazami anatazama mikono yake kama hamsikizi*)

Swai: Hata husikizi nasema nini.

Tatu: Nakusikia ...

Swai: Sasa, lakini ku ...

Tatu: Swai ... (*anamtazama*) hatuwezi kukaa kwa furaha tena baada ya haya yaliyopita.

Swai: Nimekuomba msamaha na sasa nakuomba tena – Nimekosa.

Tatu: Sio kosa lako.

Swai: Kosa lilikuwa langu sio lako lakini ...

Tatu: Si kosa lako ... kosa letu sote – kwa hiyo haina maana kukulaumu au kukuudhikia. (*Uk. 39-40*).

Tatu erkennt die Lage.

Tatu: „Tulifikiri madhali tunapendana basi inatosha - Hatukujua kuwa hata ndoa ina wakati wake“. (*Uk. 40*).

Swai möchte Tatu die Sachen mitgeben, die sie im Laufe des Ehelebens bekommen hat. Sie lehnt das Angebot ab: „Sikuja na kitu, naondoka bila kitu“ (Uk. 41). Tatu geht von der Bühne ab. Swai bleibt allein zurück.

17 Das Ehegesetz in Tansania kennt drei Arten von Eheschliessungen: *Ndoa ya Bomani*, *Ndoa ya Kidini* na *Ndoa ya Kimila*. Die *Ndoa ya Kidini* muß durch einen vereidigten Amtsvertreter (Priester, Shehe) der jeweiligen Religion bestätigt werden. Ein Exemplar des Dokumentes bleibt beim Standesamt, ein Exemplar bei der Religionsgemeinschaft und ein Exemplar beim Ehepaar. Die Gesetze der jeweiligen Religion betreffs Trennung und Scheidung gelten für sie. Für die Ehe von Swai und Tatu gelten die standesamtlichen Gesetze. Scheidung ist dabei erlaubt. Rwezaura, Balthazar A. 1981. Sheria ya Ndoa Tanzania. Dar es Salaam: TUKI. 74pp. (*B.8.13.61.*).